SEHEMU YA KUWEKA MIKONO NDANI YA SALA NA RADI KWA MAIBADHI

ALFUQAYYIR
ABUU HUDHAYFAT BN ASHUURA

بسم الله الرحمن الرحيم

Shukrani Zote Zinamstahiqi Allah Subhanahu wataala , pia Sala Na Amani Zimfikie Mtume Muhammad Na Alize Na Sahabaze , Ama Baada Ya hayo :

Zama Hizi Masuala Yamekithirika Kuhusu **Sehemu Ya Kuweka Mikono Ndani Ya Sala** , Utaskia Mmoja Anasema Kuweka Mkono Wako Wa Kulia Juu Ya Mkono Wa Kusoto Chini Ya Kitofu Ni **Uzushi** , Na Wengine Utawaona wanafunga Mikono Kwenye **Shingo** , Yote Hayo Ni Kutorudia Kwenye Kutub Na Kutokutazama Maneno Ya Wajawema Waliyotangulia , Risala Hiyi Nimeita **“ Sehemu Ya Kuweka Mikono Ndani Ya Sala Na Radi Kwa Maibadhi “** pia Risala Hiyi Imebeba Baadhi Ya Faida , Na Muomba Allah Atusamehe Tutakapokua Tumekosea Na Atuthibitishe Katika Sunna .

MTUNZI

ALFUQAYYIR ABU HUDHAYFAT BN ASHUURA .

بسم الله الرحمن الرحيم

Tambua Allah Akuhifadhi , **Mwenendo Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie Pindi Alipokua Akisali Alikua Anaweka Mkono Wake Wakulia Juu Ya Mkono Wake Wa Kusoto Ndani Ya Sala , Na Hakuna Khilafu Juu Ya Hilo Kwa Masahaba .**

Kutoka Kwa **Wail Mtoto Wa Hujr** Allah Amridhie : **" Alimuona Nabi Sala Na Amani Zimfikie Akiinuwa Mikono Yake Pindi Alipoingia Ndani Ya Sala**................. **, Kisha Akaweka Mkono Wake Wakulia Juu Ya Mkono Wake Wa Kusoto**.........**"** *Imepokewa Na Muslim 401 .*

- ***RADI KWA MAIBADHI** : " Hawainuwi Mikono Pindi Wanapoanza Sala " pia " Hawaweki Mkono Wa Kulia Juu Ya Mkono Wa Kusoto Kwa Kudai Kua Kuna Khilafu " .*

Majibu :

_ Kuinuwa Mikono Ndani Ya Sala Tumeona Hapo Juu kua Rasulullah Alikua Akiinuwa Mikono Yake Ndani Ya Sala , Na **Mtoto Wa mundhir** Kanuku " Makubaliyano ya Wanawaelimu " Anasema **Mtoto Wa mundhir : " Wamekubaliana Wanachuoni Wote Tunaowafahamu Wanasema Kuwa Mtume Sala Na Amani Zimfikie Alikua Akinyanyua Mikono Yake Anapoanza Sala , Na Ni Sehemu Ya Sunna Kwa Mtu Kunyanyua Mikono Yake Anapoanza Swala " Tazama Al Awsat 3/300 .**

_ Hakuna Khilafu Juu Ya Kuweka Mkono Wa Kulia Juu Ya Mkono Wa Kusoto Ndani Ya Sala Kama Tulivyoona Hapo Juu Kupitia Kitendo Cha Mtume Sala Na Amani Zimfikie Kuweka Mkono Wa Kulia Juu Ya Mkono Wa Kusoto , Ama Yaliyopokelewa Kutoka Kwa **Mtoto Wa Zubayr : " Kua Mtume Alikuwa Akinyoosha Mikono -**Kuto Kuweka Mkono Wa Kulia Juu Ya Mkono Wa Kusoto Ndani Ya Sala - **Pindi Anapo Sali " Sio Sahihi .**

Anasema **Tirmiziy Allah Amrehemu : " Wanachuoni Miongoni Mwa Maswahaba Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie Na Matabiina Na Waliokuja Baada Yao Wanaona Kwamba Mwanamume Anapaswa**

Kuweka Mkono Wake Wa Kulia Kwenye Mkono Wake Wa Kusoto Ndani Ya Sala " *Tazama Tuhfat 2/82 .*

Ewe Uliye Muamini Allah Subhanahu wataala , Tambua Kua **Mambo Ya Mandub -** Sunna **- Kwa Kweli Yameamriwa . Allah anasema : " Na Wala Hawakuwa Waumini Wakiume Na Waumini Wakike Pindi Allah Na Mtume Wake Wanapoamrisha Jambo Waweze Kuwa Na Khiyari……."** , Hapo Tunafaidika Kua Tusiache Mambo Ya Sunna Ao Yaliyopendekezwa .

Ni Ipi Sehemu Ya Kuweka Mikono ?

Wanawaelimu Wameikhtilafiyana Sehemu Ya Kuweka **Mikono Ndani Ya Sala Unapokua Umesimama** , Na Sababu Zinazo Fanya Wanawaelimu Kuihktilafiyana Ni :

1. **Hadith Kutokuthibiti .**
2. **Kuikhtilafiyana katika kuielewa Dalili .**
3. **Dalili Kugongana , Na Zikigongana Unatumia Njia Hizi " Kuzikusanya , Dalili Iliyovuta Nyingine , Kupima Uzito , Kuacha Zote Dalili Mbili ".**
4. **Kuikhtilafiyana Kanuni Za Usulul Fiqhi .**

Kuweka Mikono kwenye Shingo

Kutoka Kwa **Mtoto Wa Abas Allah Awaridhie Katika Tafsir pindi Allah Aliposema : " Na Usali Kwaajili Ya Mola Wako Na Uchinje " Akatafsiri**

kua “ Kuweka Mikono kwenye Shingo “ *Tazama Albayhaqi 2/31* , **Ila Ni Dhaifu .**

Bali Tafsiri Ya Aya Hiyo Ni **: “ Sema Hakika Sala Yangu Na Kichinjwa Changu Na Uhayi Wangu Na Kufariki Kwangu Ni Kwaajili Ya Allah Mola Wa Viumbe Vyote .**

Kuweka Mikono Juu Ya Kifuwa

Na Hiyi Ni **Riwaya Ya İmam Shafi Na İmam Ahmad Allah Awarehemu ,** ila Punde Tutakuja Kuona Qauli Sahihi Kuhusu Miono Yao Kuhusu Sehemu Ya Kuweka Mikono .

Anasema **Mtoto Wa Qayyum : “ Anasema Kwenye Riwaya Ya Almuzani : Mikono Inawekwa Chini Ya Kitofu Kidogo , Na Inakereheka Kuweka Mikono Juu Ya Kifuwa , Na Kwahiyo İmepokewa Kutoka Kwa Nabi Sala Na Amani Zimfikie Hakika : Yeye Amekataza - التكفير - Kuweka Mikono Juu Ya Kifuwa “** *Tazama Badai’ Alfawaid 3/92 .*

Anasema **Almarwaziy : “ Alikuwa İshaq Akitusalisha Witri…. Na Anainuwa Mikono Katika Qunut , Na Anakunut Kabla Ya Kurukuu , Na Anaweka Mikono Juu Ya Matiti , Ao Chini Ya Matiti “** *Tazama Masail 222 .*

_ Anasema Twaus : “ Alikuwa Rasulullah Sala Na Amani Zimfikie Akiweka Mkono Wa Kulia Juu Ya Mkono Wa Kusoto Kisha Anaiweka Juu Ya Kifuwa chake Na Yeye yupo Ndani Ya Sala “ *İmepokewa Na Abu Dawud 1/121 Namba 759 .*

Kanuni : Mursalu Tabi’ Siyo Hoja .

_ Hadith Wail Mtoto Wa Hujr : “ Alimuona Nabi Sala Na Amani Zimfikie Akiweka Mkono Wa Kulia Juu Ya Mkono Wa Kusoto Kisha Akaiweka Juu Ya Kifuwa “ *İmepokewa Na İbn Khuzaymah kwenye Sahih 1/243 Namba 479 , Kuna* **Muammal Mtoto Wa İsmail Ni “ Swaduk Sayi Al**

Hifdhi " ndie Aliezidisha Neno **" juu Ya Kifuwa "** Na Amekhalifu Mathiqa Waliyopokea Kwa **Sufyan Thawri hawakutaja** Neno **" Juu Ya Kifuwa " ,** ***Ziyada Hiyo ni Shadh.***

_ Hadith Qabiswah Mtoto Wa Hulb Kutoka Kwa Baba Yake Allah Amridhie Anasema : " Nilimuona Rasulullah Sala Na Amani Zimfikie Anaweka Mikono Yake Juu Ya Kifuwa chake " İmepokewa Na Ahmad 5/226 Na Tirmiziy 2/32 Na İbn Madjah 1/226 , Kuna **Qabiswah Mtoto Wa Hulb " Hajulikani " , Wengine Wakasema Ni " Swaduk "** Lakini Ametafarrud, pia Waliyopokea Kutoka Kwa **" Simak Mtoto Wa Harb " wamoja wamepokea Kwa Matamshi : " Juu Ya Kifuwa " Na Wengine Wakapokea " Bila Matamshi Ya Juu Ya Kifuwa " ,** Kwahiyo Hadith Hiyi **İnaugonjwa .**

Utofauti Wa Mwanamke Na Mwanamume Sehemu Ya Kuweka Mikono

Hanafiyah Wanaona Mwanamke Anaweka Juu Ya Kifuwa , Na Mwanamume Anaweka Chini Ya Kitofu , *Tazama Fathul Qadir Cha Ibn Himam 1/249-250 .*

Kuweka Mikono Juu Ya Kitofu

Ni Riwaya Ya **Malik Na Shafi' Na Ahmad Allah Awarehemu , Nawawiy Amerajihisha Katika Madhebu Ya Shafi kwenye Majmu' 3/313 .**

Anasema **Mtoto Wa Abdulbari Allah Amrehemu : " Anasema Ahmad Mtoto Wa Hanbal : Juu Ya Kitofu , Na Niqauli Ya Said Mtoto Wa Jubayr , Na Anasema Ahmad Mtoto Wa Hanbal : Na İkiwa Chini Ya Kitofu Hakuna Tatizo "** *Tazama Tamhid 20/75 .*

Kuweka Mikono Chini Ya Kitofu

Riwaya Ya **Shafi' "** *Tazama Tuhfatul Ahwadhiy 2/83 " ,* **Na Ahmad Na Ndio Rajih Kwa Madhehebu "** *Tazama Al İnswaf 2/46 " .*

Kutoka Kwa Ali Allah Amridhie Anasema : " Hakika Katika Sunna Ndani Ya Sala Ni Kuweka Kiganja Juu Ya Kiganja Chini Ya Kitofu " *İmepokewa Na Ahmad 1/110 Na Abu Dawud 1/480 , Kuna* **Abdurrahman Mtoto Wa İshaq Alwasitwiy** Ni **Dhaifu .**

Anasema Al Aynil Hanafiy Allah amrehemu : " Hiyi Ni Qauli Ya Ali Mtoto Wa Baba Twalib Na İsnad hiyo Mpaka Kwa Mtume Sala Na Amani Zimfikie Sio Sahih " *Tazama Umdatul Qariy 5/279 .*

Kunyoosha Mikono huku Umesimama

Ni **Madhehebu Ya İmam Malik , Na Ni Kinyume Na Dalili Aliyoashiria İmam Malik Katika Kuonesha Sheriya Ya Kufunga Mikono Ndani Ya Sala "** *Tazama Muwatwa Mlango Kuweka Mkono Juu Ya Mungine Ndani Ya Sala " .*

Anasema **Assindiy Allah Amrehemu : " Na Haqi Haikuthibiti Hadith Sahihi Juu Ya Kunyoosha Mikono Ndani Ya Sala "** *Tazama Fathul Khafur 60 .*

Na Wengine **Katika Malikiya Ni Ruhsa Kufunga Mikono Ndani Ya Sala Ya Nafila Pekee .**

- Ama kuhusu **İmam Malik Kukereheka Na Kitendo Cha Kufunga Mikono ,** Na Kusema Kua **Hakijui , Anasema Mtoto Wa Azzuz :**

_ Anasema Mtoto Wa Qassim : Nikamuuliza Malik Kuhusu Mtu Anasali Huku Ameegamiya Ukuta , Akasema Malik : Katika Sala Za Fardhi Hainistaajabishi , Ama Katika Sala Za Nafila Sioni Kama Kuna Tatizo , Anasema Mtoto Wa Qassim : Na Akijishkiza Fimbo Mkononi Mwake , Akasema Malik : Akitaka Atajishkiza Na Asipotaka Hatojishkiza , Na Alikua İmam Malik Hakerahiki Kujishkiza Fimbo ,........Na Akasema Malik Kuweka Mkono Wa Kulia Juu Ya Mkono Wa Kusoto Ndani Ya Sala , Sijui Jambo Hilo Katika Sala Za Fardhi , Na Alikua Akikereheka Kuweka Mkono Wa Kulia Juu Ya Mkono Wa Kusoto Ndani Ya Sala ,

Lakini Ndani Ya Sala Za Nafila İkiwa Atarefusha Kisomo Hakuna Tatizo kuegamia Mkono Wa Kulia Juu Ya Mkono Wa Kusoto............, **Kukereheka Kwa Alivyopokea Mtoto Wa Qassim Ni Kwa Kuweka Mkono Wa Kulia Juu Ya Mkono Wa Kusoto Kwakukusudia Kuegamia …… “** *Tazama Rasail Bn Azzuz 42-43 .*
** *Tunafaidika Kua Ni Sheriya Kuweka Mkono Wa Kulia Juu Ya Mkono Wa Kusoto Ndani Ya Sala, Na İmam Malik Alikereheka MTU Akisali Akaegamiya kwa Kufunga Mkono Wa Kulia Juu Ya Mkono Wa Kusoto Ndani Ya Sala.*

_ **Ama İmam Malik kusema “ Sijui Hilo “ :** Anakusudia Kua **Sijui Kama Ni Katika Wajibu Wa Ndani Ya Sala ,** kama Alivyofanya Ta’wil **Mtoto Wa Rushdi** Qauli Ya **Malik** kwenye **Mudawwanah** : **Sijui Qauli Ya Watu Kwenye Ruku: Subhana Rabi Al Adhim , Na Kwenye Sijida : Subhana Rabi Al A’la , Na Akapinga , Anasema Mtoto Wa Rushdi : Amepinga Kua Maneno Hayo Ni Lazima Kuyaleta Ndani Ya Sala** “ *Tazama Albayan Watahswil 1/361 “ .*

Anasema Mtoto Wa Azzuz : “ Tasbih kwenye Rukuu Na Sujud Anasema İmam Malik Kuhusu Tasbih Hizo: “ Sizijuwi “ Kanakwamba Anaashiria Kauli Ya Baadhi Ya Waimam Waliyotangulia Kuhusu Ulazima Wa Tasbih Kwenye Rukuu Na Sujud (Hajui Ulazima Wa Tasbih Kwenye Rukuu Na Sujud) Mpaka Madhehebu Ya Ahmad Mtoto Wa Hanbal Wanaonao Kuacha Tasbih Hizo Kwa Makusudi Sala İnaharibika “ *Tazama Rasail Bn Azzuz 44 .*

Utakapo Njoo Utaweka Mikono “ Chini Ya Kifuwa Ao Juu , Na Chini Ya Kitofu Ao Juu “

Anasema **Mtoto Wa Mundhir Allah Amrehemu : “ Haikuthibiti chochote Juu Ya Hayo Kutoka Kwa Mtume Sala Na Amani Zimfikie , Anakhiyari -** *MwenyeKusali -* **“** *Tazama Naylul Awtwar 2/189 .*

Anasema **Tirmiziy Allah Amrehemu : " Wanachuoni Miongoni Mwa Maswahaba Wa Mtume Sala Na Amani Zimfikie Na Matabiina Na Waliokuja Baada Yao Wanaona Kwamba Mwanamume Anapaswa Kuweka Mkono Wake Wa Kulia Kwenye Mkono Wake Wa Kusoto Ndani Ya Sala , Na Wengine Wakaona : Ataweka Mikono Juu Ya Kitofu , Na Wengine Wakaona : Ataweka Mikono Chini Ya Kitofu , Na Hayo Yote Kwao Ni Wasaa** - Pana - **"** *Tazama Sunan Tirmiziy 2/82 .*

***** Na Ndio Qauli Yenye Nguvu .***

Kipengele

Kutoka Kwa Abdillah Mtoto Muslimah, kutoka kwa Malik , kutoka Kwa Baba Hazim , Kutoka Kwa Sahl Mtoto Sa'd Allah Amridhie Anasema : " **Watu Waliamrishwa Kuweka Mkono Wao Wa Kulia Juu Ya Mkono Wao Wa Kusoto Ndani Ya Sala " Baba Hazim Anasema : Mimi Sijui İspokua - يَنمي - Kwamba Sahl Mtoto Sa'd Allah Amridhie Anaegamiza Kwa Mtume Sala Na Amani Zimfikie ,** *İmepokewa Na Bukhari Na Malik .*

- ***RADI KWA MAIBADHI:*** *" Wanadai Kua Baba Hazim Hiyo ni Zana Yake Kusema Hivo " Na Wakasema " Law Kama İngelikuwa İmeinuliwa Haingehitajika Baba Hazim Kusema Hajui İspokua….."*

Majibu :

_ Law Hangesema **Baba Hazim : Mimi Sijui İspokua Kwamba Sahl Mtoto Sa'd Allah Amridhie Anaegamiza Kwa Mtume Sala Na Amani Zimfikie ,** İngelikuwa İmebeba **" حكم المرفوع - İko Na Hukmu İliyoinuliwa Kwa Mtume Sala Na Amani Zimfikie " ,** *Sababu Qauli Ya Sahaba: Tulikuwa Tunaamrishwa Kadha , Hiyi İnatuonesha Kua Muamrishaji Ni Mtume Sala Na Amani Zimfikie.*

_ pia **Abu Hazim Alitaka Kuweka Wazi , Sababu** Neno **“ Watu Waliamrishwa “** Hiyi Haiyitwi : مرفوع İliyoegamizwa Kwa Mtume Sala Na Amani Zimfikie , Bali İnaitwa : حكم المرفوع Hukmu İliyoinuliwa Kwa Mtume Sala Na Amani Zimfikie .

Hitimisho :

1. **Utakapo Msalia Mtume Sala Na Amani Si Sheria Kuweka Mkono Wako Kifuwani Ao Rohoni .**
2. **Hadith Ya Mtu Ambae Apendezeshi Sala Yake Hata Kama Mtume Sala Na Amani Zimfikie Hakumwambia Aweke Mkono Wa Kulia Juu Ya Mkono Wa Kusoto, vile vile Hakumwambia Alete Tasbih Za Rukuu Na Sujud , Na Tashahud Kubwa Na Ndogo , Na Sami' Allah liman Hamida , Na Rabana Walakal Hamdu , Na Kutowa Salam , Kumbe Asije Mtu Na Kutumia Hadith Hiyi Kwakukataza Kuweka Mkono Wa Kulia Juu Ya Mkono Wa Kusoto , Sababu Tutamlazimisha Asilete Ambavyo Mtume Sala Na Amani Zimfikie Hakumfundisha Sahaba Huyo .**
3. **Ama Hadith ya Mtume Kuwakataza Masahaba Wasiinuwe Mikono Yao Pindi Wanapotowa Salamu ndani Ya Sala Kama Mikia Ya Farasi , hiyi Hamkatazi Mtu Kuinuwa Mikono Yake Anapofungua Sala Yake Na pindi Anaporuku Na Pindi Anapotoka kwenye Rukuu Na Pindi Anaposimama Kutoka Rakaa Ya pili Na Kuanza Ya Tatu .**

Allah Anasema : “ Sema İkiwa Nyinyi Mnampenda Allah Nifwateni Mimi Allah Atakupendeni Na Atakufutieni Madhambi Yenu . Na Allah Ni Mwenye Kufuta Madhambi Na Mwenye Kurehemu “ *Suratul Al İmran Aya Ya 31 .*

سبحانك اللهم وبحمدك أشهد أن لا إله إلا أنت أستغفرك وأتوب إليك.

SEHEMU YA KUWEKA MIKONO NDANI YA SALA NA RADI KWA MAIBADHI

ALFUQAYYIR
ABUU HUDHAYFAT BN ASHUURA